



**LOWELL PUBLIC SCHOOLS**  
Henry J. Mroz Central Administration Offices  
155 Merrimack Street  
Lowell, MA 01852

Oktoaba 9, 2020

Wapenzi Familia wa Lowell Public Schools,

Katika siku ya Jumatano, tuligawa nanyi idadi za mwisho kabisa kutoka ripoti ya dashibodi ya wiki ya jimbo ya COVID-19 na namna idadi za maradhi za COVID-19 katika Lowell zinaendelea kuongezeka. Kulingana na taarifa ya mwisho ya Jumatano hii, kiwango cha wastani katika watu 100,000 wa Lowell kila siku ni 16.3, ambalo ni ongezeko kutoka idadi ya 10.9 wiki iliyopita. Hili linaliweka mji wa Lowell katika alama “nyekundu” ama kikundi cha “hatari ya juu” katika wiki ya pili inayofuata. Kiwango chetu “cha asilimia cha maradhi” (asilimia ya vipimo zinazopata maradhi katika mgonjwa katika hapa Lowell) ziliongezeka kutoka 3.57%, kutoka 2.71% katika wiki iliyopita.

Idara ya Masomo ya Shule ya Msingi na Shule ya Upili imewashauri wilaya za shule kuendelea kutathmini data za wiki tatu zinazofuatana kutoka Ripoti ya Wiki ya Afya ya Umma ya COVID-19 kutoka Jimbo Huru. Mnamo Oktoba 8, 2020, Bodi la Afya la Lowell lilitoa mwongozo kwamba “wiki tatu katika alama nyekundu ni sababu ya kutosha kuzingatia mafunzo ya mbali.” Kwa hivyo, tulitaka kuwapatia familia kumbukumbu ya kutosha iwezekanavyo kwamba **iwapo Lowell tena itapatiwa alama “nyekundu” wiki ifuatayo, wilaya itabadilisha mkondo kwa muundo wa mafunzo ya mbali kikamilifu kuanzia mwanzo wa shule Jumatatu, Oktoba 19, 2020.** Tutaendelea kuchunguza uwezekano za kipekee kwa programu maalum ndogo zaidi na tutaendelea kuwasiliana kuhusu uwezekano wowote wa kipekee wiki ijayo baada ya kutathmini data mpya ya COVID-19.

Tangu mwanzo wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi, tumekuwa na tukio chache pekee za COVID-19 ndani ya shule zetu; lakini hii ni hatua ya kinga ya kiafya tukizingatia viwango vya sasa vya uambukizi wa kijamii wa sasa wa COVID-19 ndani ya Lowell. Tunafahamu athari maamuzi haya magumu yalizo nazo kwa wanafunzi na familia, kwa hivyo barua hili linakusudia kupea habari mapema iwezekanavyo kabla ya ufunuzi wa data wa wiki ijayo. Katika nokta hii, Lowell imewekwa kwa alama “nyekundu” kwa wiki mbili pekee, kwa hivyo **mafunzo ya kuhudhuria darasani yataendelea wiki ijayo kama ilivyopangwa.** Tutawasiliana nawe asubuhi ya Alhamisi ijayo huku tukiwa na taarifa zaidi na baada ya kutathmini data ya mwisho kabisa iliyotolewa na Idara ya Afya na Ripoti ya Wiki ya Afya ya Umma ya COVID-19 kutoka Jimbo Huru.

Asante sana kwa ushirikiano wako unaoendelea na urahisi wa kubadilika huku tukifanya bidii ili kulinda usalama wa wanafunzi, familia, na wafanyikazi wetu katika muda huu mgumu na usiyoweza kujulikana.

Wako Mwaminifu,

John J. Leahy  
Meya

Dr. Joel D. Boyd  
Msimamizi wa Mashule